**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE UFUNGUZI WA MAONESHO NA SHEREHE ZA WAKULIMA, WAFUGAJI NA WAVUVI - NANENANE

**VIWANJA VYA MAONESHO NZUGUNI – DODOMA**
**01 AGOSTI, 2025**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...**

Napenda kuanza hotuba yangu kwa kuwasilisha kwenu salamu za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye anawapongeza na kuwashukuru sana wakulima, wafugaji na wavuvi nchini kote kwa kazi nzuri ambayo licha ya kulihakikishia Taifa usalama wa chakula, inawezesha pia upatikanaji wa ajira na kipato, malighafi za viwanda, fedha za kigeni na kukuza uchumi wa nchi yetu. Vilevile, nawashukuru na kuwapongeza waandaaji wa maonesho haya ya 32 Kitaifa, kwa maandalizi ya kiwango. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Hussein Bashe (Mb), Waziri wa Kilimo; Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi; Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; Halima Dendego, Mkuu wa Mkoa wa Singida; viongozi na watumishi wa Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Taasisi za Umma na Binafsi; Washirika wa Maendeleo na Wananchi wote wa kanda ya kati kwa kufika kwa wingi kushiriki katika maonesho na sherehe za Nanenane 2025 kitaifa, tunayofungua leo hapa Dodoma.

***Ndugu Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wananchi;***

Maonesho haya yanaadhimishwa kitaifa katika Kanda ya Kati hapa Jijini Dodoma na katika Kanda saba (Mbeya, Morogoro, Tabora, Arusha, Lindi, Mwanza, na Bariadi). Lengo la maonesho haya ni kutoa fursa kwa Wakulima, Wafugaji, Wavuvi, Wadau wote wa kilimo-biashara, Wanaushirika na wadau wengine, kubadilishana uzoefu na kujifunza teknolojia za kisasa za kilimo, ufugaji na uvuvi, kupata fursa za masoko ambazo ni endelevu na zenye kuleta tija; kusambaza matokeo ya tafiti na teknolojia bora.

***Ndugu Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wananchi;***

Sekta za kilimo, mifugo na uvuvi zimekuwa mhimili muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa letu na kuleta maendeleo kwa wananchi. Mathalan, katika mwaka 2024 sekta hizi zimeendelea kuimarika na kuchangia 26.3% (zaidi ya ¼) katika Pato la Taifa. Sekta ndogo ya kilimo cha mazao imechangia 16.1% ya Pato la Taifa, mifugo (6.2%) na uvuvi (1.7%). Aidha, Sekta hizi zimetoa ajira kwa wastani wa 61.4% ya idadi ya Watanzania wote, na kuwezesha upatikanaji wa zaidi ya 60% ya malighafi za viwanda na kuhakikisha nchi inakuwa na usalama wa chakula. Mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi yameendelea kuwa chanzo muhimu cha fedha za kigeni kutoka Dola za Marekani Bilioni 1.2 mwaka 2019/2020 hadi Dola za Marekani Bilioni 3.54 mwaka 2023/2024. Mauzo haya ni matokeo ya jitihada za wakulima katika kuongeza uzalishaji wa mazao kutoka tani milioni 17.15 (2021/2022) hadi tani milioni 22.8 (2023/2024). Aidha, Kitaifa Tanzania inajitosheleza kwa chakula ikiwa na uwiano wa kujitosheleza kwa chakula wa 128% (*food self sufficieny ratio*). Pia, nchi yetu inauza ziada nje, hasa mahindi, mchele na korosho katika nchi jirani zinapokuwa na uhaba wa chakula. Kwa niaba ya Serikali, nawapongeza sana wakulima, wafugaji, wavuvi, wananchi wanaojihusisha na kilimo-biashara, viwanda vya kuchakata mazao, pamoja na wadau wengine wote wa kilimo kwa mafanikio haya na kwa kuendeleza sekta hii muhimu. Kwa hakika ninyi ni fahari ya Tanzania.

***Ndugu Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wananchi;***

Umuhimu wa kilimo nilioueleza na mafanikio yaliyopatikana yametokana na juhudi mbalimbali za wakulima, wafugaji, wavuvi, wadau wa maendeleo, pamoja na jitihada mahususi za Serikali inayoongozwa na Dkt Samia Suluhu Hassan katika kukuza sekta hii. Jitihada za dhati za Serikali ni pamoja na kuongeza bajeti za Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi, pamoja na sekta nyingine saidizi. Katika bajeti ya 2025/2026 Wizara ya kilimo imetengewa Shilingi Trilioni 1.243, ikilinganishwa na Shilingi Bilioni 229.99 mwaka 2021/2022. Vilevile, Wizara ya Mifugo na Uvuvi nayo imetengewa Shilingi Bilioni 476.6 ikilinganishwa na Shilingi Bilioni 169.2 mwaka 2021/2022. Hatua nyingine mahsusi ni pamoja na kuongeza upatikanaji wa ruzuku za pembejeo; kuimarisha upatikanaji wa mitaji na kuhimiza maendeleo ya ushirika; kuwezesha upatikanaji wa huduma za ugani na zana bora za kilimo; kujenga miundombinu ya kuhifadhi mazao na kutafuta masoko ya mazao na bidhaa za kilimo. Kwa upande wa mifugo na uvuvi, Serikali iliongeza bajeti za kufanya tafiti kuhusu uzalishaji wa mbegu bora; udhibiti wa magonjwa ya mifugo; utambuzi wa mifugo; uzalishaji wa mbegu za malisho; ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia mazao na masoko; ukuzaji wa viumbe maji, uchumi wa buluu na miradi ya kuwezesha vijana; kuchimba malambo kwa ajili ya kunywesha mifugo; kununua zana bora za uvuvi, zikiwemo boti n.k. Aidha, Mhe. Rais mwenyewe alizindua kampeni ya Kitaifa ya chanjo na utambuzi wa mifugo (16 Juni, 2025). Tunamshukuru sana Mhe. Rais na Serikali yake kwa jitihada zote hizi ambazo zimeleta matokeo chanya katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, pamoja na sekta saidizi kwa maendeleo ya kilimo kwa ujumla wake.

***Ndugu Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wananchi;***

Zipo changamoto kuu zinazoathiri na kuchelewesha maendeleo ya sekta ya kilimo na mifugo hapa nchini. Changamoto hizo ni pamoja na, kutozingatia kanuni za kilimo bora (*inefficient farming practices*); teknolojia duni na ukosefu wa mitaji (*limited technology and finance*); miundombinu isiyotosheleza mahitaji, hususan miundombinu ya umwagiliaji, kuhifadhi mazao, barabara za vijijini, umeme n.k.; athari za mabadiliko ya tabianchi hususan ukame/mafuriko zinazofanya uzalishaji kuwa mdogo; na, ukosefu wa masoko. Japokuwa Kitaifa nchi yetu inajitosheleza kwa chakula, yapo baadhi ya maeneo na kaya masikini ambazo zinakumbwa na uhaba wa chakula kutokana na kwamba kilimo chetu bado kinategemea mvua, pamoja na matumizi kidogo ya teknolojia za kisasa za kilimo. Aidha, inakadiriwa kuwa zaidi ya robo ya Watanzania wanaishi chini ya kiwango kinachotakiwa cha mahitaji ya msingi (*basic needs*). Vilevile, 35% ya watoto chini ya umri wa miaka 5 wana udumavu kutokana na lishe duni. Changamoto nyingine zinahusu ubora, upatikanaji na upotevu wa chakula baada ya mavuno. Kwa upande wa mifugo na uvuvi, changamoto ni tija ndogo, mapato yasiyowiana na wingi wa mifugo tuliyonayo nchini, na kushindwa kutumia fursa kubwa tuliyonayo ya uvuvi katika bahari kuu na Maziwa makuu, ufugaji wa viumbe maji na mazao ya misitu na nyuki.

***Ndugu Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wananchi;***

Kama tulivyoelezwa, maonesho ya Nanenane ya mwaka 2025 yanaongozwa na Kaulimbiu isemayo ***"Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo,***

***Mifugo na Uvuvi 2025".*** Kaulimbiu hii imechaguliwa mahsusi ili kutukumbusha umuhimu wa viongozi bora katika kuinua uzalishaji kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi, hasa katika kipindi hiki tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuuu, Oktoba 2025. Aidha, kwa kuzingatia kaulimbiu hii na changamoto nilizokwisha kuzieleza, napenda kutumia fursa hii kusisitiza mambo yafuatayo, nikijikita zaidi kuwakumbusha viongozi wa sasa na watakaochaguliwa kuhusu wajibu mkubwa tulionao katika kukuza maendeleo ya kilimo, mifugo, uvuvi na sekta saidizi.

**Kwanza,** viongozi tunao wajibu wa kuetekeleza dira ya 2050 iliyozinduliwa hivi karibuni na mipango ya maendeleo ya sekta ya kilimo, inayotaka kuongeza kasi ya ukuaji wa kilimo hadi kufikia 10% kwa mwaka, ifikapo 2030 na kuendelea. Hivyo, viongozi tuna wajibu wa kuhakikisha tunaifanya Tanzania kuwa kitovu cha chakula katika ukanda wa Afrika, na kusimamia mageuzi yanayohitajika kufikia malengo hayo. Pamoja na mambo mengine, tunawajibika kuwaelekeza wakulima, wafugaji na wavuvi wetu kuweka nguvu zaidi kwenye mazao yenye thamani kubwa sokoni; kuwekeza katika uzalishaji wa kisasa wa bidhaa zinazotokana na mifugo ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje; kuendeleza uvuvi na ufugaji wa samaki; kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika miundombinu baridi ya uhifadhi na usafirishaji; kujiimarisha zaidi katika kilimo-biashara, kuhamasisha uwekezaji mkubwa katika teknolojia za kisasa za kilimo, ikiwemo kilimo-janja; uwekezaji katika umwagiliaji; upatikanaji wa fedha na mitaji; na kutafuta masoko ya uhakika.

**Pili,** viongozi wanahimizwa kusimamia uwezeshaji wa wakulima, wafugaji na wavuvi kiuchumi, hususan upatikanaji wa mitaji, teknolojia, elimu na mafunzo, pamoja na upatikanaji wa huduma za ugani, ikiwemo kukuza matumizi ya kanuni bora za kilimo.

**Tatu,** viongozi wahamasishe maendeleo ya ushirika na ushirikiano kati ya wakulima/wafugaji/wavuvi na watafiti, maafisa ugani na watunga sera. Jambo hili litawezesha kubadilishana na kuchangiana elimu/ujuzi, rasilimali, mbinu bora na mifano halisi ya kuongeza tija.

**Nne,** viongozi wote wanao wajibu wa kuhimiza utekelezaji wa sera na mikakati inayowezesha kilimo kukua kwa haraka zaidi, hususan uwekezaji katika miundombinu wezeshi, utafiti na elimu. Pia, utekelezaji wa sera zinazowezesha kilimo-biashara ili kutengeneza faida na kumlinda mkulima.

**Tano,** ni wajibu wa viongozi kuhimiza wananchi wetu kutumia mbinu zinazoweza kuhimili athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi na changamoto nyingine zinazowakumba wakulima. Hii ni pamoja na kuhimiza matumizi bora ya ardhi, kushawishi wananchi kupanua mawanda ya kilimo (*diversification*) na kuhimiza zaidi kilimo cha mazao yanayohimili ukame.

**Sita,** viongozi tunapaswa pia kuweka mkazo katika kujenga nguvukazi na rasilimaliwatu yenye ubora kwa maendeleo ya kilimo, kwa kutilia mkazo mafunzo kwa vitendo kwa wakulima na wataalam wa kilimo. Aidha, ni wajibu wa viongozi kujenga na kuendeleza taasisi za kilimo ikiwemo ushirika na vyama vya wakulima.

**Saba,** viongozi makini tunao pia wajibu wa kufuatilia na kupima matokeo ya utekelezaji wa mipango na miradi ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Aidha, tumieni matokeo ya ufuatiliaji na tathmini kuelekeza rasilimali ili zitumike kwa tija zaidi na kufikia malengo.

**Nane,** viongozi mnawajibika kutoa elimu kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wasindikaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kuhusu fursa zilizopo za kupata mitaji kutoka kwenye Benki zetu kama NMB, CRDB, TADB na Taasisi nyingine za fedha ambazo tayari zinatoa mikopo nafuu kwa ajili ya kilimo-biashara. Aidha, fanyeni jitihada za kuwaunganisha na makampuni ya teknolojia kama SIDO, Vyuo Vikuu na Taasisi za ufundi zinazobuni teknolojia rahisi na nafuu, zikiwemo za kuchakata na kuhifadhi mazao kwa ajili ya kuongeza tija katika sekta hizi.

***Ndugu Wakulima, Wafugaji , Wavuvi na Wananchi;***
Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwashukuru kwa mara nyingine tena wakulima, wafugaji, wavuvi na wote wanaojishughulisha na kilimo-biashara, na viwanda vinavyochakata mazao ya kilimo hapa Tanzania kwa mchango wenu adhimu katika maendeleo ya nchi yetu, usalama na uhai wa Watanzania. Aidha, asanteni sana wote mliofika katika viwanja hivi vya Nzuguni kushiriki uzinduzi wa Nanenane 2025 kitaifa na kutembelea mabanda ya maonesho. Ninawaalika Watanzania katika mikoa ya ukanda wa kati kutenga muda kutembelea maonesho haya hadi yatakapofikia kilele. Hakika mtavuna maarifa makubwa yanayohusu maendeleo ya sekta hizi muhimu sana.

Baada ya kusema hayo, sasa ninayo heshima kutamka kuwa Maonesho na Sherehe za Wakulima, Wafugaji na Wavuvi (Nanenane) 2025, yamefunguliwa rasmi.

**Wakulima, Wafugaji na Wavuvi Oyee!**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**